

Ndugu Familia za FCPS:

Kwa utekelezaji wa matriki ya FCPS COVID-19 ya kujifunza kwa kibinafi, tuliahidi kufanya maamuzi wiki mbili mapema na kutangaza maamuzi kila Jumanne [siku ya pili] ili kuwapa jamii yetu muda wa kutosha kujitayarisha.

Wanafunzi wa chekechea, darasa la kwanza na la pili walitakiwa kuwa vyuoni wiki za Februari 16-19 na Februari 22-26, lakini tuliposhiriki kabla ya hapo, wanafunzi wote watajifunza kwa mbali wiki hii kwa sababu ya hali ya hewa. Moja ya sababu tulijumuisha wiki mbili kwa awamu yetu ya kwanza ilikuwa kuhakikisha tuna wafanyakazi kusaidia awamu zinazofuata.

Uhakiki leo wa deta pamoja na Idara ya Afya ya Kata ya Lexington-Fayette ulionyesha kuwa Wastani wa Siku 7 wa kesi mpya umeshuka hadi 100, ambukizo katika jamii inazidi kupunguka, kesi kati ya watoto wenye umri wa kwenda shule zinapunguka, na wafanyakazi wetu wengi wamepokea kipimo cha pili cha chanjo.

Kuanzia leo tunaweza:

- Thibitisha kuwa wanafunzi wa chekechea, darasa la kwanza na la pili ambao familia zao zilichagua kujifunza kwa kibinafsi zitarudi chuoni wiki ya Februari 22-26, hali ya hewa ikiruhusu, na kuendelea kujifunza kwa kibinafi wiki ya Machi 1-5, 2021 .
- **Tangaza kwamba tunatarajia kuwa na wanafunzi katika madarasa ya 3-5 ambao familia zao zilichagua kusoma kwa kibinafsi kurudi chuoni Machi 3-5, 2021.** (Uamuzi huu utakaguliwa na kuthibitishwa Jumanne [siku ya pili] ijayo.)
- Thibitisha kuwa tunachunguza hali nyingi tofauti ili kutimiza lengo la kutoa majifunzo kwa kibinafsi kwa wanafunzi wote ambao familia zao zimechagua chaguo hilo.
- Sisitiza umuhimu wa mambo ya mabadiliko, pamoja na kupatikana kwa madereva wa basi na wafanyakazi wa mkahawa, tunapopangia viwango vingine vya darasa kurudi na kujifunza kwa kibinafsi katika njia yetu polepole.
- Kumtia moyo mtu yeyote ambaye anaweza kupenda kufanya kazi kama dereva wa basi, mfuatiliaji wa basi, au mfanyakazi wa lishe ya watoto kuomba kwenye www.fcps.net/jobs.

Asante kwa kuendelea kusaidia na kwa kutuelewa.